**102/3**

**KISWAHILI**

**FASIHI**

**KARATASI YA 3**

**JULAI /AGOSTI 2014**

**MUDA : SAA 2 ½**

For More Free KCSE Past Papers Visit www.freekcsepastpapers.com

# MTIHANI WA MWIGO WA KAUNTI NDOGO YA NYAMIRA

***Hati ya kuhitimu kisomo Sekondari Kenya(KCSE)***

**102/3**

**Kiswahili**

Karatasi ya 3

**Saa 2 ½**

**MAAGIZO:**

- *Andika **jina lako** na **nambari yako katika** nafasi ulizoachiwa hapo juu*
- *Jibu maswali **manne pekee.***
- *Swali la **kwanza** ni **lazima.***
- *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizosalia yaani; (Riwaya, Hadithi fupi, Tamthiliai na, fasihi simulizi.*
- ***Usijibu** maswali mawili kutoka sehemu moja*
- *Kila swali lina alama **20***

***KWA MATUMIZI YA MTAHINI :-***

| **Swali** | **Upeo** | **Alama** |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| **Jumla** | **80** | |

*Karatasi hii ina kurasa **3** zilizopigwa chapa.Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo*

## SEHEMU YA A: USHAIRI

## SWALI LA LAZIMA

**1.** ***Soma shairi kisha ujibu maswali yafuatayo***

Walimwengu nambieni,
Mie nipate fahamu
Hawamo vijana wetu
Meingilia yapi mambo,
Hulkazo hawa wana, tewengu zatia waj,
Sampuli ya hivi vikembe,
Lipi jama nelimisha

Watembea kwa vihindo
Mirindimo ardhi tia,
Ole wako kikutana, nao hawa masultani,
Takupita ja risasi, vikumbo nusura upigwe,
Wanadi maisha ni shoti
Wapapie kwa haraka

Viatu vya chuchumia, ati mbingu wafikila,
Magotini vyabisha hodi, waungwana waole,
Vishati vya kuninginia,
Matumboni ja kima,
Waso haya wana haa,
Wana mji wao ati,

Kikutana nao njinai,
Manywele taambani, maashiki wa rasta,
Bbmal waabudu, ndio jagina wao wana,
Ziki lao la kisasa, lashangaza weni waja,
Sautiyo maskio,
Kusikiza ole wako, tajipata umepokewa,

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

Na hapa jahazi, langu ufukoni lafikile,
Enyi vijana pilika,
Ya kisasa kufuata,
Bila hadhari si haki,
Tuchuje yenye tijara,
Ya izara tupuzile,
Heshima tudumishe, tamaduni tuienzi.

For More Free KCSE Past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Kwa kutoa mifano, eleza mambo mshairi analalamikia (al.3)

(b)Eleza ukitoa mifano namna utungo huu umezingatia kaida za ushairi kimuundo (al.3)

(c) Andika mfano moja wa (al.4)

(i) Mstari mishata

(ii) Mstari kifu

(d) Eleza namna uhuru wa ushairi unavyodhihirika katika utungo huu

(e) Andika ubeti wan ne kwa lugha tutumbi (al.4)

(e)Andika toni ya shairi hii (al.2)

(i) Libasi

(ii) Tijara

**SEHEMU YA B: RIWAYA**

**KIDAGAA KIMEMWOZEA- KEN WALIBORA**

***Jibu swali la pili au la tatu***

2. Dhuluma ni jambo la kawaida katika jumuia ya kidagaa kimemwozea. Jadili (alama.20)

3. ………………….unaa…………seema mimiiiiii sipakui ?.......................wataka mimi nipike ?

Ehee ? Ati mimi nalaza damu ? Wewe unaiamsha damu ?

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili

(b) Eleza mbinu zozote tatu za lugha zilizotumika katika dondoo hili (alama.6)

(c) Jadili ufaafu wa anwani kwa kurejelea mnenaji (alama.10)

**SEHEMU YA C. TAMTHILIA**

**MSTAHIKI MEYA-TIMOTHY AREGE**

***Jibu swali la 4 an 5***

4. "Ninalotaka kusema ni kwamba sikumbuki kushiriki…….ongezeko hilo……….

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama.4)

(b) Eleza matokeo ya mazungmzo haya (alama.6)

(c) Onyesha jinsi onezeko hili linadhihirisha tamaa ya viongozi katika baraza la cheneo (alama.10)

5. Eleza namna asasi zifuatazo zinavyoendeleza maovu dhidi ya umma (alama.20)

(i) Dini

(ii) Nchi za magharibi

(iii) Baraza la mji

(iv) Idara ya polisi

**SEHEMU YA D-HADITHI FUPI**

**DAMU NYEUSI-KEN WALIBORA S.A MOHAMMED**

***Jibu swali la 6 au la 7***

6. Maovu katika jamii ni maudhui yasioyoshughulikia pakubwa katika diwani ya Damu Nyeusi na hadithi nyinginezo. Thibitisha kwa kurejelea

(i) Smaki wa nchi joto

(ii) Damu nyeusi

(iii) Gilasi ya mwisho makaburini

(iv) Maeko

(v) Kanda la usufi

7. " Alitembea kando ya barabara kwenye kijia cha wapiti njia huku akinyapianyapia nyapu nyapu na kupepesuka pepesu pepesu kama mlevi chakari."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama.4)

(b) Eleza sifa za anayerejelewa (alama.8)

(c) Mhusika huyu ana umuhimu gani katika hadithi (alama.6)

(d) Eleza mbinu mili ambazo zimetumiwa katika dondoo hili (alama.2)

**SEHEMU YA E. FASIHI SIMULIZI**

8. (a) Eleza maana ya ngomezi (alama.2)

(b) Eleza sifa za ngomezi (alama.4)

(c) Toa mifano ya ngomezi katika maisha ya kisasa (alama.4)

(d) Maghani ni nini? (alama.4)

(e) Fafanua maana ya vipera hivi vya fasihi simulizi

(i)vivugo (alama.2)

(ii) tondozi (alama.2)

(iii) Pembezi (alama.2)

(iv) Rara (alama.2)

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com